**JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**JESHI LA POLISI TANZANIA**

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## RUHUSA KWA MABASI YA ABIRIA KUANZA KUPATIWA RATIBA YA KUSAFIRI KWA SAA 24 KUANZIA JUMAPILI TAREHE 01.10.2023

**Ndugu Wanahabari,** itakumbukwa kwamba mwaka 1994 Serikali ilizuia mabasi ya abiria kusafiri usiku. Zuio hilo lilisababishwa na matukio ya utekaji wa mabasi uliohusisha uporaji na udhalilishaji wa abiria, ajali mbaya za mabasi zilizogharimu Maisha ya watu na wengine kupata ulemavu wa kudumu na uharibifu wa mali na miundombinu ya barabara. Utekaji wa mabasi ulikuwa unafanyika kwenye maeneo yaliyokuwa na barabara mbovu na ambayo hayakuwa na mawasiliano ya simu.

**Ndugu Wanahabari,** sote tumeshuhudia kuwa changamoto za usalama na miundombinu zilizokuwepo kipindi cha miaka ya 90 zimepungua sana au kuondolewa kabisa kutokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Miundombinu ya barabara na mawasiliano ya simu vimeimarishwa karibu maeneo yote nchini. Mwaka 2019, Serikali kupitia Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, iliruhusu mabasi yote kukamilisha safari zake bila kujali ukomo wa muda wa saa 6.00 usiku isipokuwa kwenye maeneo yenye viashiria vya matishio ya kiusalama.

**Ndugu Wanahabari,** Kutokana na usikivu wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwishoni mwa Mwaka 2022, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ilianzisha ratiba za kuanza safari saa 11.00 alfajiri

badala ya 12.00 muda ambao ulikuwa umezoeleka tangu Mwaka 1994. Aidha, mwezi Mei, 2023 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilitoa ridhaa ya kiusalama kwa LATRA kuanza kutoa ratiba za kuanza safari saa 09.00 usiku. Tathimini iliyofanyika kufuatia mabadiliko haya ya ratiba imeonyesha kuna mwitikio mkubwa wa wananchi kutumia mabasi hayo yanayoanza safari mapema na hakujajitokeza tatizo lolote baya la kutishia usalama.

**Ndugu Wanahabari,** kwa ujumla juhudi za Jeshi la Polisi katika kupambana na kudhibiti uhalifu ikiwemo kufanya doria katika barabara kuu na barabara za Mikoa; hatua ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kutekeleza Mfumo wa Ufuatiliaji Mwenendo wa Mabasi ya Abiria (VTS) kwa saa 24 pamoja na LATRA kuanza kutekeleza Kanuni ya Kuthibitishaji Madereva na Kusajili Wahudumu wa Vyombo vya Usafiri Kibiashara ya Mwaka 2020, zimesaidia kupunguza matukio makubwa ya ajali za barabarani.

**Ndugu Wanahabari,** Mfumo wa VTS unaotekelezwa na LATRA umeunganishwa pia katika vituo vya Jeshi la Polisi – Kikosi cha Usalama Barabarani, na kwa sasa Wakuu wa Usalama wa Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara na Mikoa Maalum ya Kipolisi (RTOs) pamoja na Wakuu wa Usalama Barabarani Wilayani (DTOs) wameunganishwa kwenye Mfumo huu na waaweza kufuatilia mwenendo wa mabasi ya abiria kwa saa 24/7. Madereva waliothibitishwa na LATRA wamepatiwa vitufe vya utambuzi (*identification button* au *i-button*) ambavyo wanapaswa kuvitumia wakati wote wanapoendesha gari au kubadilishana gari baada ya kuendesha kwa saa 8. I-buton inawezesha LATRA na Jeshi la Polisi kujua dereva anayeendesha basi wakati wote wa safari.

**Ndugu Wanahabari,** kufuatia mabadiliko hayo chanya na dhamira ya Serikali kuimarisha shughuli za uchumi wa Wananchi wake wa maeneo ya mjini na vijijini, kwa kuzingatia maoni ya wadau mbalimbali wakiwemo Wabunge, wamiliki wa mabasi, madereva wa mabasi, wasafiri, wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla, Serikali iliamua kuondoa zuio la mabasi ya abiria kusafiri nyakati za usiku lililowekwa mwaka 1994. Akitoa Hoja ya Kuahirisha Mkutano wa 11 wa Bunge la bajeti tarehe 28 Juni, 2023, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu, aliziagiza, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kuweka utaratibu wa mabasi kusafirisha abiria nyakati za usiku.

**Ndugu Wanahabari,** kufuatia uamuzi huo, Wizara zetu mbili zilianza mara moja kutekeleza Agizo la Mhe. Waziri Mkuu kuruhusu magari ya abiria kuanza safari zao kuanzia saa 9:00 usiku huku zikiendelea kufanya tathmini za kiusalama kwenye njia zingine zote. Tathmini yetu imeonesha kwamba:

a) Udhibiti wa usalama kupitia Jeshi la Polisi umeimarishwa kutokana na jitihada za Serikali ya Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
b) Mwamko wa wananchi, hususan wafanya biashara kutumia taasisi za kifedha badala ya kusafiri na fedha taslimu (cash) umeongezeka.
c) Serikali imeimarisha huduma za mawasiliano ya simu kwa kujenga minara ya mawasiliano kwenye maoneo mengi nchini.
d) Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inao Mfumo madhubuti wa Kufuatilia Mwenendo wa Mabasi (VTS) unaofanyakazi kwa saa 24.
e) Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi imeboresha miundombinu ya usafiri, hususan barabara kuu na barabara za mikoa na hivyo kufanya Nchi

yetu kuwa moja ya Nchi zenye usafiri wa barabara unaoaminika na bora.

f) Wafanyabiashara wengi wanaomiliki mabasi ya abiria walio tayari kufanya safari za saa 24 wako tayari pia kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo kuhusu usafiri na usafirishaji wa abiria.

**Ndugu Wanahabari,** kwa msingi wa Hoja hizo hapo juu na kwa dhamira ya dhati aliyonayo Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuona mazingira ya kufanya biashara Nchini yanakuwa bora na kuimarisha shughuli za kiuchumi miongoni mwa Watanzania na Wawekezaji, Serikali inatangaza kuanza rasmi kutolewa kwa ratiba za mabasi ya abiria kusafiri kwa saa 24 kuanzia tarehe 01 Oktoba, 2023.

Katika kutekeleza uamuzi huo, wenye nia njema, yafuatayo yanapaswa yazingatiwe na wadau wote wa usafiri na usafirishaji wakiwemo wamiliki wa mabasi, abiria, madereva, LATRA, TANROADS, TAMISEMI na Jeshi la Polisi:

a) Wamiliki wa mabasi wanapaswa kuhakikisha yafuatayo:

   Waombaji wa ratiba wanatakiwa kuwa na angalau mabasi manne (4) yaliyo kwenye hali nzuri, kuhakikisha wanazingatia masharti yote ya leseni za usafirishaji yakiwemo yanayohusiana na madereva wao na kuanisha vituo maalumu vya kubadilishana madereva kwa safari zinazozidi umbali wa kilomita 800. Dereva wa pili atatakiwa kusubiri kwenye kituo cha kubadilishana kitakachoainishwa. Aidha, mizigo yote itatakiwa kuwekewa alama ya utambulisho na orodha ya abiria kutolewa kwa njia ya elektroniki.

b) Abiria wanapaswa kutekeleza yafuatayo:

Kuhakikisha wanakataka tiketi kwa njia ya elektroniki na taarifa zao zinaandikwa kwa usahihi, kutoa taarifa kwa uvunjaji wowote wa kanuni kwa kupiga simu LATRA (bure) 0800 11 00 19 au 0800 11 00 20 au kupiga simu ya polisi namba 0682887722 au 0658444499.

c) Maderewa wa mabasi wanapaswa kuhakikisha yafuatayo:

Madereva wote watatakiwa kuwa amethibitishwa na LATRA na kutumia kitufe cha utambuzi (i-button), kuzingatia sheria ya usalama barabara hususan mwendo na matumizi sahihi ya barabara na kujali haki za abiria.

d) LATRA wanatakiwa kutekeleza yafuatayo:

Kuanza kutoa ratiba za safari za usiku kwa kushirikisha watoa huduma, kuhakikisha Mfumo wa VTS na kituo cha mawasiliano vinafanyakazi wakati wote (24/7) na kutoa elimu kuhusiana na haki za abiria na majukumu ya watoa huduma zinazodhibitiwa.

e) TANROADS ijielekeze kuhakikisha majukumu yafuatayo:

Ubora wa miundombinu ya Barabara, uwepo wa alama na michoro ya barabarani, uondoshaji wa haraka wa magari mabovu barabarani na kutoa elimu kwa umma kuhusiana na utunzaji wa miundombinu.

f) TAMISEMI wanapaswa kusimamia yafuatayo:

Kuhakikisha kunakuwepo na usalama wa abiria na huduma za msingi kwenye stendi zote.

g) Jeshi la Polisi watapaswa kutekeleza majukumu yao ya msingi pamoja na haya yafuatayo:

Kuimarisha doria katika maeneo ya stendi, barabara kuu na Barabara za mikoani ili kudhibiti uhalifu unaoweza kutokea na kuchukua hatua stahiki kwa madereva watakaokiuka Sheria za Usalama Barabarani ikiwa ni pamoja na kuwafungia leseni madereva sugu.

Kwa kumalizia, niwaelekeze Jeshi la Polisi kutumia Mfumo wa VTS kutoa namba ya malipo (control number) kwa madereva na wamiliki ambao magari yao yatakuwa yanakwenda mwendo kasi mkubwa usiku.

Mwisho, Serikali inataka kuona kuwa usafiri kwa saa 24 unakuwa salama na wenye ufanisi. Hilo linawezekana endapo kila mmoja atatimiza wajibu wake.

**Asanteni Sana**

**MHE. JUMANNE A. SAGINI (MB)**
**MWENYEKITI WA BARAZA LA TAIFA LA USALAMA BARABARANI**
**29 SEPTEMBA, 2023**